

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

KUFUNGA KWA NJIA INAYOLINGANA NA MAFUNDISHO YA BIBLIA

"Ikiwa Wakristo watafunga huku wakiwa na moyo safi na nia safi, jambo hilo linaweza kuwa ufunguo ambao utafungua milango ambayo haiwezi kufunguliwa na funguo za aina nyininge yote; pia linaweza kuwa dirisha ambayo italeta mwangaza unaoangazia mbali sana katika ulimwenguni ambao hauonekani; na inaweza kuwa silaha ya kiroho yake Mungu ambayo, 'ina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome.'" —Arthur Wallis

Kufunga katika Agano la Kale na Agano Jipyä

Kufunga kupitia kwa kujinyima chakula ni jambo ambalo lilitfundishwa na kufuatwa na watakatifu katika Agano la Kale na Agano Jipyä. Kihistoria, inajulikana kwamba wake na waume ambao walikuwa shupavu kwa mambo ya kiroho walikuwa wakijifunga kula chakula. Baadhi ya watu hao ni Musa (ambaye ndiye alileta sheria), mfalme Daudi, nabii Eliya, Malkia Esta, nabii Danieli, nabii (mwanamke) Ana, Yesu Mwana wa Mungu, na hata mtume Paulo. Kwa kweli kufunga ni njia ya mtu kufungua akili na roho yake na kunyenyeka mbele zake Mungu, jambo ambalo linamwezesha kushirikiana na Bwana kwa njia ya karibu zaidi katika mambo ya kiroho. Walakini, katika historia, kufunga kulibadilika na kufanyika kuwa ni jamboa la mtu kujionyesha kwa watu wale wengine kwamba yeye ni mtu wa kiroho. Ukweli ni kwamba mazoea ya watu wa kisasa ya kufuata mambo ya kale bila kuzingatia maana yake haijawahi kuwa njia bora ya kumwezesha mtu kumkaribia Mungu. Katika juhudhi zote za mwanadamu za kujitoa kwa Mungu, mambo yote ambayo anatenda na ambayo yanaweza kuonekana na wanadamu mwenzake huwa ni chanzo cha kupata nguvu za kiroho kwa kulingana na jinsi roho ya mtu huyo ilivyo na tamaa ya kumpendeza Mungu kwa unyenyekevu na utakatifu. Yohana Wesley akasema kwamba, "Watu wengine wametukiza tendo la kufunga kwa ajili ya dini na kulifanya lifikie kiwango ambacho kamwe hakilingani na Maandiko, wala kuambatana na akili timamu za mwanadamu; ingawa nao watu wengine wamefanya makosa ya kupuuzilia mbali jambo hili la kufunga." Lakini ukweli ni kwamba kuna mazoea ya kufunga ambayo yanalingana na biblia na ambayo ni ya manufaa makubwa kwa watoto wa Mungu hata katika siku hizi zetu.

Maana Kamili ya Neno Kufunga

Neno "kufunga" limepewa maana nydingi, na watu wengi wamelipatia maana ya kuwa ni tendo la mtu kuamua kujinyima mambo ya kimwili. Lakini hata ingawa Wakristo

wana haja ya kuwa wenye kiasi, na pia kuwa watu wanaotawala tamaa zao za kimwili, neno "kufunga" (kama linavyopatikana katika Biblia), lina maana hasa ya tendo la mtu kuamua kujinyima chakula. Basi ni muhimu kwamba tusipunguze au kuongezea maana zaidi katika urahisi wa maana hiyo, ya kwamba ni mtu kujinyima chakula cha kimwili.

Ishara ya Kuomboleza

Kufunga ilikuwa ni ishara ya maombolezo, ya kuonyesha masumbufo ya kiakili, ya kuonyesha majonzi. Wakati mfalme Sauli alikufa Daudi alifunga hadi jioni (2 Samueli 1:11-12), na watu wale wengine nao wakafunga kwa kipindi cha siku saba kuonyesha maombolezo yao na heshima yao kwa Sauli (1 Mambo ya Nyakati 10:11-12).



"Kwa kweli kufunga ni njia ya mtu kufungua akili na roho yake na kunyenyeka mbele zake Mungu, jambo ambalo linamwezesha kushirikiana na Bwana kwa njia ya karibu zaidi katika mambo ya kiroho."

Kufunga kwa Ajili ya Upatanisho Katika Sheria

Katika sheria ya Musa kufunga siku moja katika "Siku ya Upatanisho" ilikuwa ndio kufunga kwa pekee ambako kuriamriwa na Mungu na ambako kulifanya kwa mazoea na watu hadharani. "Itakuwa kwenu sabato ya kustarehe kabisa, nanyi mtazitesa nafsi zenu; siku ya kenda ya mwezi wakati wa jioni, tangu jioni hata jioni, mtaishika hiyo Sabato yenu" (Walawi 23:26-32). Maneno "kutesa nafsi zenu" ni jambo ambalo liliashiria mtu kujinyima chakula. Ilikuwa ni ishara ya maombolezo na mtu kunyenyeka roho yake mbele zake Mungu. Mfalme Daudi alisema kwamba aliadhibu roho yake kwa kufunga (Zaburi 69:10). Katika Siku ya

(Endelea katika Ukurasa 2)

Makala:
Kufunga kwa Njia
Inayolingana na
Mafundisho ya Biblia

Tahariri
Aina Nne za Kufunga

Mafundisho ya Biblia:
Kufunga

4

Maswali na Majibu
Kuingizwa Kwenye
Tafsiri za Biblia
Maneno Ambayo
Hayakuwemo Mbeleni

7

Je, Wajua?
Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

Upatanisho kufunga kuliambatana na watu kutoa sadaka na ilikuwa siku ambayo watu hawakufanya kazi. Nao Wayahudi wa Agano Jipywa waliendelea na mazoea hayo ya kufunga katika Siku hiyo ya Upatanisho (Matendo 27:9).

Sherehe Nne za Wayahudi za Kila Mwaka

Zaidi ya siku hiyo ya kufunga, ambapo maneno ya Bwana yalisomwa (Yeremia 36:6), kulikuwa na sherehe zingine nne ambazo Wayahudi walisherehekeea hadharani kama kumbukumbu ya siku ambayo mji wa Yerusalem uliangamizwa (Zekaria 8:19). Lakini kando na siku hizo tano tendo la watu kufunga katika Agano la Kale lilikuwa ni jambo la kibinasi, isipokuwa iwe kwamba kuna haja maalum ambayo imeibuka na ambayo imefanya kuwe na mwito wa watu kufunga hadharani. Basi rekodi hiyo ya watu kufunga katika Agano la Kale ni chanzo bora cha mafundisho kuhusu nguvu na kusudi ya jambo hilo katika siku hizi zetu.

Kufunga kwa Pamoja Hadharani

Mara ya kwanza ambako kufunga kwa pamoja hadharani kama ni sherehe ya kidini ilikuwa ni tukio lile ambalo limenakiliwa katika Waamuzi 20:26. Wana wa Israeli walikuwa vitani na wakaja katika nyumba ya Mungu "na kulia, wakaketi hapo mbele za Bwana, wakafunga siku hiyo hata jioni." Mungu naye akaingilia kati katika hali hiyo, kwa ajili yao, na akawapa ushindii. Pia, wakati mfalme Yehoshafati alilemewa na mambo ambayo yalikuwa yamemkumba yeye alimililia Mungu wakati ambapo taifa la Yuda lilipovamiwa. "Akatangaza mbiu ya watu kufunga katika Yuda yote" na watu wakaja kumtafuta Mungu na kumwomba msaada wake wa kiungu (2 Mambo ya Nyakati 20:2-7). Na katika kuitikia maombi yao ya dhatti Mungu akawaambia ya kwamba: "Msiogope, wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu... simameni, mkaune wokovu wa Bwana" (2 Mambo ya Nyakati 20:15-18).

Nguvu Zinazopatikana kwa Kumwitia Mungu

Nguvu za mtu kumwitia Mungu kwa njia maombi ya kufunga zinaonekana wakati Wayahudi walikuwa Babiloni na wakatishwa na tangazo kwamba wangeuawa. Malkia Esta alitoa mwongozo wa kuwaongoza Wayahudi kukusanya pamoja "mkafunge kwa ajili yangu; msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana" (Esta 4:16-17). Mungu naye aliheshimu tendo hilo la kufunga na kufanya watu wake kuonyeshwa huruma. Naye Ezra na mahame wenzake wakati wakirudi Yerusalem walikumbwa na safari iliyo kuwa hatari. Lakini badala ya kumwomba mfalme kuwapa askari wa kuwalinda Ezra akasema "Basi tukafunga, tukamsihi Mungu wetu kwa ajili ya hayo; naye akatutakabali" (Ezra 8:21-23). Mungu akajionyesha kwamba anaheshimu maombi yanayoandamana na kufunga.

Kufunga kwa Njia ya Kibinasi

Mfalme Daudi alikuwa na utaratibu wa kufunga kwa njia ya kibinasi. Yeye alinyenyekenza nafsi yake kwa njia ya kufunga (Zaburi 35:11-13) ili aweze kumtafuta Mungu kwa maombi yenye ari zaidi. Baada ya Daudi kutenda dhambi na Bathsheba mtoto wake alingonjeka hadi

(Endelea katika Ukurasa 5)

Gazeti la Ukweli wa Injili ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tudembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tarayi ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la Ukweli wa Injili linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@gospeltruth.org

Tahariri



Nikamwelekeza Bwana Mungu uso wangu, ili kusihu kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvala nguo za magunia na majivu. —Danieli 9:3

Kama ingekuwa kwamba wanaume na wanawake wa sasa ambao wanamcha Mungu wangeelekeza nyuso zao kwa Bwana na kumtafuta kwa kuomba na kufunga mimi nina uhakika kwamba wao wangkuwa wa kiroho zaidi, wenye upako zaidi, na wenye nguvu zaidi ndani yake Mungu. Somo letu robo hii ya mwaka linahusiana na swala la kufunga. Kufunga ni jambo ambalo limetumiwa vibaya na kuweza kutolelewka na watu wengi, na kwa sasa ni jambo ambalo ni nadra sana kupatikana kati ya watakatifu.

Kufunga si jambo la mtu kujiadhibu, na pia sio jambo la mtu kumlazimisha Mungu ili kupata kile anatamani. Kufunga ni tendo la toba, la mtu kunyenyeka ili kumheshimu Bwana huku akiwa na nia ya kujitenga na chakula ili kuweka umuhimu maswala yake Mungu. Sisi sote tuna shughuli nyingi katika maisha yetu ya kila siku, ndiposa kufunga ni wakati bora wa mtu kupunguza mwendo, kusafisha akili zake, kujiweka wakfu mbele zake Bwana. Jambo hili huzidisha ushirika wa kiroho na kutufanya sisi kuwa watu walio karibu sana na Mungu. Matokeo yake ni kwamba Bwana anapata mweke wa kufanya kazi na kujidhihirisha kwa njia ya kibinagsi zaidi. Kufunga kwa kufuata njia ilio ya ukweli ni mweke wa Wakristo kubadilisha matukio ya kawaida ya kidunia kwa kutumia nguvu za Mungu wakati yeye ameingilia kati kwenye matukio hayo.

Mimi mwenyewe nimepata changa moto ya kibinagsi kupitia kwa maandiko ambayo yanahusiana na somo hili. Ni ombi langu kwamba sisi sote tutamtafuta Bwana ili tuweze kuelewa zaidi, tuwe waaminifu zaidi, na tuweze kujitoa zaidi kwa jambo hili la kufunga.

—Michael Smith
Julai 2018



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujianidikisha na

kupata jarida

za mbele.

AINA NNE ZA KUFUNGA

KUFUNGA KWA NGUVU ZA KIUNGU

Kufunga ambako mtu huweza kufanya kupitia kwa nguvu za Mungu.

Musa alifunga kwa vipindi viwili vyaa siku 40. Kumbukumbu 9:9, 18.
Eliya hakula siku 40. 1 Wafalme 19:8

KUFUNGA KWA NJIA YA KAWAIDA

Kujitenga na chakula lakini kuendelea kunywa vinywaji.

Kufunga ambako Yehoshafati alifanya. 2 Mambo ya Nyakati 20:3
Daudi alijitenga na chakula. 2 Samueli 12:21
Yesu hakula, lakini kuna uwezekano kwamba Yeye alikuwa akinywa.
Mathayo 4:2

KUFUNGA KABISA KABISA

Pasipo kula au kunywa kitu chochote

Watu na wanyama wa Ninewi hawakula au kunywa. Yona 3:5-10
(Ezra 10:6)
Kujifunga kula na kunywa. Esta 4:15-16
Sauli hakula au kunywa. Matendo 9:9

KUFUNGA NUSU-NUSU

Kujizua kula chakula cha wakati fulani au kufunga aina fulani ya chakula.

Danieli hakula vinono na nyama. Danieli 10:2-3

Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: KUFUNGA

Somo la Biblia: *Takaseni saumu, iteni kusanyiko la dini, wazee na wakusanye wenyeji wote wa nchi; waende nyumbani kwa BWANA, Mungu wenu, na kumlilia BWANA.* —Yoeli 1:14

Muhstasari: Kufunga ni jambo ambalo tangu jadi limekuwa likifuatwa na watu wa Mungu katika Agano la Kale na Agano Jipy, na ni sehemu muhimu ya maisha ya Mkristo wa kisasa. Hili ni tendo ambalo Mkristo hufanya la kuonekana mwilini; ni tendo la mtu kujinyima kimwili; tendo ambalo linawenza kusaidia akili, mwili, na roho ya mtu ili ziweze kuwa makini zaidi kwa mambo ya Mungu. Hii ni njia ya mtu kupata nguvu zake Mungu ambazo huleta ukombozi, mwongozo, kumwagiwa mafuta, na hata kumwezesha mtu kukua kiroho.

Maana yake: Hata ingawa ni vizuri Wakristo kujinyima katika fani mbali mbali maishani mwao, neno "kufunga" hasa linamaanisha mtu kujitenga na chakula.

I. Kufunga kumeamriwa katika Sheria ya Musa

- A. Walawi 23:26-32 "Siku ya upatanisho" ilikuwa ni siku pekee ya kufunga ambayo iliamriwa katika sheria (Walawi 16:29-31; Hesabu 29:7).
- B. Maana ya "Kutesa nafsi zenu" ni kufunga.
- C. Zaburi 69:10 Daudi aliadhibu roho yake kwa kufunga.
- D. Matendo 27:9 Wahayudi wa Agano Jipy waliendelea kufunga katika Siku ya Upatanisho.

II. Aina Nne za Kufunga Ambazo Zilifanywa Kila Mwaka Katika Agano la Kale

- A. Zekaria 28:19 Sherehe nne za kila mwaka zilitumiwa kusherehekeea matukio makubwa ambayo yalihuishwa na kuanguka kwa mji wa Yerusalem.

III. Nyakati na Sababu za Kufunga katika Agano la Kale

- A. 1 Mambo ya Nyakati 10:12 Wakati wa kifo na majonzi (2 Samueli 1:11-12).
- B. 2 Samueli 12:16-23 Daudi alifunga wakati mtoto wake alipokuwa mgonjwa.
- C. Zaburi 35:11-13 Daudi alitesa nafsi yake kwa kufunga.
- D. Nehemia 9:1-3 Tendo la kuungama dhambi wakati sheria ilikuwa ikisomwa (Yeremia 36:6).
- E. Waamuzi 20:25-26 Katika wakati wa vita (1 Samueli 7:5-8).
- F. 2 Mambo ya Nyakati 20:3 Yehoshafati alifunga wakati taifa la Yuda lilipovamiwa.
- G. Ezra 8:21,23 Wale waliohamishwa walifunga ili kupata usalama katika safari yao.
- H. Esta 4:3,16 Ili kuokolewa kutokana na tangazo la kifo.
- I. Kumbukumbu la Torati 9:17-20 Musa alifunga kwa ajili ya dhambi ya wana wa Israeli.
- J. Danieli 9:3-5 Danieli alifunga huku akikiri dhambi za wana wa Israeli.

- K. 1 Wafalme 21:17-29 Ahabu alifunga ili asamehewe.

- L. Yona 3:4-10 Ninewe, ili kubadilisha kauli lake Mungu.

IV. Mafundisho na Mfano wake Kristo

- A. Mathayo 4:1-9 Yesu alifunga katika nyakati zake za majoribu na kwa sababu ya maandalizi ya huduma yake.
- B. Mathayo 6:5, 16-18 "Wakati" utakapofunga, wala sio "kama" utafunga.
- C. Mathayo 9:14-17 Siku sijazo wanafunzi wa Yesu watakuwa wakifunga.
- D. Marko 9:17-29 Kupata nguvu na imani zaidi kwa kufunga na kuomba (Mathayo 17:14-21).

V. Kufunga katika Kanisa la Agano Jipy

- A. Luka 2:37 Kabla ya wakati wa Yesu kufika Ana alikuwa "akiabudu na kufunga."
- B. Matendo 9:9 Sauli alifunga kwa siku tatu.
- C. 2 Wakorintho 6:4-10 Paulo alifunga mara nyingi.
- D. Matendo 13:1-3 Kanisa la Antioikia lilifunga lilipokuwa likituma mishenari.
- E. Matendo 14:21-23 Makanisa ya Wagalatia wakati yakiwawekea wazee mikono kwa utumishi wake Bwana.

VI. Kufunga Ambako Kunakubalika na Kusikokubalika

- A. Isaya 58:3-6 Kufunga kwa ajili ya sherehe tu, na kwa njia ya kimwili, bila ya mtu kutubu kwa njia ya ukweli ni jambo ambalo halikubaliki.
- B. Zekaria 7:1-14 Kufunga bila ya mtu kuwa mtiifu au bila kutafuta utukufu wake Mungu hakufai kwa vyoyoyote vile.
- C. Mathayo 6:16-18 Kufunga kwa kulingana na urahisi na unyenyekevu wake.
- D. Yoeli 2:12-13 Kwa moyo wako wote.

Tamati

Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi; ndipo watakapofunga. —Mathayo 9:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 2)

kufa: "Mtoto alipokuwa hai, nalifunga, nikalia; . . . Lakini sasa amekufa nifungie nini?" (2 Samueli 12:15-23).

Kufunga kwa Ajili ya Toba

Kufunga ni jambo ambalo liliambatanishwa na mtu kutubu mbele zake Mungu. Musa alifunga siku arobanne (usiku na mchana) kwa ajili ya dhambi ya watu wake (Kumbukumbu 9:18). Naye Mungu akamwokoa Ahabu kutokana na hukumu ambayo alikuwa ametangaza wakati Ahabu alipotubu na kunyenyeyekeza moyo wake kwa njia ya kufunga (1 Wafalme 21:27-29). Watu wa Ninewe nao waliamini hukumu zake Mungu kama ziliviotangazwa na Yona na wakafunga (pamoja na wanyama wao) na kumtafuta Mungu ili abadilishe mawazo yake. Naye Mungu akaheshimu kufunga na toba yao na akabdalisha hasira yake kwao (Yohana 3:5-10).

Daniel naye alielekeza uso wake kwa Bwana "kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga" (Danieli 9:3). Akatoa maisha yake kwa Mungu ili kumwomba rehema kwa ajili ya dhambi za watu wake. Na ni katika kipindi hicho cha kufunga ndipo nabii Gabrieli alipojitokeza kwake na kumpatia unabii wa ajabu na uwezo wa kuelewa maswala zaliyohusiana na Masihi ambaye angekuja (aya ya 21-23).

Hata ingawa kufunga silo jambo ambalo (wakati mwingi) liliamuriwa na Mungu katika Agano la Kale, lakini ni jambo ambalo lilitumiwa na watu wa Mungu walipokumbwa na shida na matatizo tofauti. Wao walifunga ili kupata msamaha wa dhambi, walipokuwa wagonjwa, na pia wakati wakivamiwa na adui. Pia wakafunga kwa ajili ya kunyenyeyekeza roho zao mbele zake Mungu na ili kutafuta msaada wake wa kiungu, kupata faraja yake, na ili kwamba Yeye aingilie kati.

Mifano Kutoka kwa Agano Jipy

Hata wakati ambapo Mafarisayo walifanya tendo la kujinyima chakula kuwa kifungo cha kiroho, kuna watu ambaa waliendelea kufunga huku wakiwa na roho ya kutaka kumtukuza Mungu. Hata kabla ya Kristo kuanza huduma yake nabii Ana alikuwa "haondoki katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba" (Luka 2:36-37).

Katika maandalizi ya huduma yake, Yesu "alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa" (Mathayo 4:1-3). Hebu tuzingatie kwamba Musa alifunga siku arobanne kabla ya kupokea sheria kutoka kwa Mungu. Naye Eliya, ambaye alikuwa mwakilishi wa manabii, alifunga siku arobanne; na hata Kristo, ambaye ndiye mwanzilishi wa Agano Jipy, pia alifunga siku arobanne. Na ingawa hii ndio rekodi ya pekee ya Kristo kufunga, Yeye alituachia mfano wa mtu ambaye ameyejinyima chakula cha kimwili ili kuweza kunywa zaidi kutoka kwa kikombe cha kiroho cha huduma ya Injili ambayo ilikuwa mbele yake. Ndiposa Yeye akapata mizizi na nguvu dhidi ya vita ambavyo vilikuwa mbele yake, na hata dhidi ya majoribu, kutokana na wakati wake wa kufunga na kumwomba Mungu.

Yesu Alifundisha Kuhusu Kufunga Lakini Sio kwa Njia ya Moja kwa Moja

Hata ingawa kufunga silo jambo lilioamuriwa katika Agano Jipy, Yesu alifundisha kuhusu jambo hilo, na pia likawekewa mkazo kwa yale ambayo mitume na kanisa la kwanza walifanya. Yesu akasema, "Tena mfungapo . . ." (Mathayo 6:16). Yeye hakusema, "Ikiwa mtafunga . . ." Yeye alijua kwamba wasikilizaji wake walijua mazoea na umuhimu wa mtu

kufunga. Ilikuwa imeeleka kwanba kufunga ni sehemu ya maisha ya mtu wa Mungu ambaye amejitoa kwake Mungu.

Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji walikuja kwa Yesu na kumuuliza: "Kwa nini sisi na Mafarisayo twafunga, bali wanafunzi wako hawafungi?" Yesu akawajibu, "Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi; ndipo watakapofunga" (mstari wa 15). Ni kweli kwamba wanafunzi wa Yesu hawakufunga mara nyingi kama Wayahudi wale wengine, jambo ambalo lilizua maswali akilini mwa watu wale wengine. Ingawa kuna mafundisho mengi ambayo yamezuka kutokana na andiko hilo, kwenye urahisi wake, andiko hilo linaonyesha kwamba Yesu hakuwa amefungwa na sheria yoyote iliyohusiana na haja ya mtu kufunga. Wakati Yesu alikuwa na wanafunzi wake wao hawakuwa na haja ya kujinyima chakula kwa sababu walikuwa katika uwepo wake Mfalme; lakini baada ya Yeye kurudi kwa Baba "ndipo watakapofunga." Kusema kweli baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni kuna rekodi kwamba kanisa lilifunga ikiwa moja ya njia ya wao kujitoa kumtafuta Mungu.



Kwa Ajili ya Kupata

Nguvu za Mungu

Kuna wakati mmoja ambapo wanafunzi wa Yesu walishindwa kumtoa pepo kutoka kwa mtoto. Yesu naye akachukua fursa hiyo kuwafundisha kuhusu umuhimu wa imani na akawaambia, "Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga" (Mathayo 17:14-21; Marko 9:17-29). Kulingana na maandiko ambayo tumeyaangalia hapo mbeleni wakati huo wanafunzi hawakuwa na utaratibu wa kufunga, hata ingawa wao waliweza kutoa pepo wachafu na kuponya wagonjwa. Basi hapa Yesu alikuwa akitilia mkazo umuhimu wa imani. Akaonelea kwamba huo ulikuwa ni wakati bora wa kufundisha, huku akisema kuhusu wakati ambaa ungekuja ambapo Yeye hatakuwa nao mwilini. Akawaonyesha kwamba imani ambayo walihitaji ili wawe na nguvu za aina hiyo ingepatikana tu kuperti kwa mtu kuwa na uhusiano wa karibu zaidi na wa kiroho na Mungu, uhusiano ambaa ungepatikana tu kuperti kwa kufunga na kuomba.

Mtume Sauli Alifunga

Baada ya Yesu kujidhihirisa kwa Sauli hapo katika njiani ya kuelekea Dameski, Sauli alipewa jukumu la kupeleka injili kwa watu wa Mataifa. Jambo la kwanza ambalo Sauli alifanya ilikuwa kufunga kwa siku tatu (Matendo 9:9). Wakati huu ndio ulikuwa wa maandalizi kwa ajili ya huduma na wa kupata upako wa kiungu maishani mwake. Baadaye mtume Paulo alijidhihirisha kuwa mhuduma wa kweli wa Mungu kuperti kufunga sana (2 Wakorintho 6:4-10). Yeye aliweka kando mambo ya mpito na ya kimwili ya maisha haya na kujitoa mhanga kumtafuta Mungu ili kupata nguvu na upako wake.

Kanisa la Kwanza Linatafuta Mwongozo

Wakati kanisa la Antioquia ilikuwa likimwambudu Bwana "na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha

(Endelea katika Ukurasa 6)

waende zao" (Matendo 13:2-3). Huu ni mfano bora wa kanisa la kwanza likifunga na kuomba. Ni wakati huu ndipo Roho Mtakatifu alitoa wito wa kiungu kwa ajili ya manufaa ya huduma. Na kupitia kwa kufunga na kuomba tena watu hao wakawekewe mikono walioitwa ili wapate nguvu za kiungu. Nalo kanisa la Wagalatia likawakeea wazee wa kanisa lao wakfu kwa njia ya kufunga na kuomba (Matendo 14:23). Basi ni ombi langu kwamba watu wa Mungu katika nyakati hizi zetu watakuwa na mzigo na ukakamavu huo kuhusiana na wito wa Mungu maishani mwao.



Kufunga lilikuwa ni dhihirisho la kweli la uzito ambao kanisa la kwanza lilichukulia hitaji lao la kupata mwelekeo na mwongozo wa Roho Mtakatifu katika jambo hili. Kama basi kanisa la leo linataka kupata nguvu na upako kwa jinsi kanisa la kwanza liliyopata, na pia kupata vipawa vya Kiroho, itabidi kanisa la kisasa

kujitoa kwa kiwango hicho hicho katika ukweli na shauku ya kumtafuta Roho Mtakatifu."

tamaduni ya kale ya kujionyesha kwamba yeye ni mtu wa kiroho, ukweli ni kwamba, kufunga kunatakiwa kuwa ni sehemu ya maisha ya mtu ambaye amejitoa kwake Mungu. Kufunga ni tendo la mtu kujiamulia kibinagsi, na ambalo chanzo chake kinastahili kuwa ni Roho wake Mungu. Ni jambo ambalo linastahili kutokana na mtu kutambua kwamba yeye ana haja kubwa ya Mungu kufanya kazi maishani mwake. Kwa kweli kuna wakati ambapo Wakristo watahitaji kufunga kwa pamoja kama kusanyiko, kama ambavyo watu wa kale walivyofanya. Jambo kama hilo linastahili kufanyika wakati ambapo watu wa Mungu wametambua kwamba wana hitaji la pamoja. Watu wa Mungu wanapoungana pamoja katika maombi na kufunga, huku wakinyenyekea mbele zake Mungu kwa pamoja, Shetani hana budi kutetemeka. Basi wakati wa kufunga ni wakati ambapo mtu huweka mawazo yake na mwili wake kwa mambo ya Mungu, na kujinyima mambo ya mwili, ili aweze kutilia maanani mambo ya kiroho.

Lakini kufunga sio kitu cha mtu kutumia ili kumlazimisha Mungu kufanya jambo fulani, na pia sio tendo la mtu kususia chakula ili kumshurutisha Mungu. Kufunga ni ishara na shauku la kusudi la kweli. Inaweza pia kuwa ni ishara ya unyenyekevu, na ni nafasi ya mtu kutafuta nguvu zake Mungu. Pia inaweza kuwa ni mweke wa kumwezesha mtu kukua kiroho, na ni wakati ambapo Roho wa Mungu anaweza kujidhahirisha ili kutoa mwongozo na upako kwa kiwango ambacho hakiwezi kupatikana kwa njia ingine yoyote ile.

Kufunga Kunahitaji Kufanya

Huku Mtu Akiwa na Nia Safi

Kufunga kuna manufaa, mradi tu kumefanya kutokana na mhusika kuwa mtiifu huku akiwa na moyo wa ukweli na ulio wazi. Mungu aliwakemea wana wa Israeli katika Isaya 58:3-6 kwa ajili ya kufunga huku wakiwa na roho mbaya. Wana wa Israeli walikuwa wakiuliza, "Mbona tumefunga?" kwa sababu walikuwa wakifunga lakini Mungu hakuwa akiwajibu. Naye Mungu akawaambia kwamba sababu ya wao kufunga ilikuwa ni "kushindana na kugombana." Wao walikuwa wakifunga kwa kimwili, huku wakifuta shauku na tamaa zao wenyewe. Kwa kweli hawakuwa wamejitelea wala kunyenyekoa mbele zake Bwana. Basi ikawa kwamba Mungu hakubali kufunga walikokuwa wakifanya. Ni jambo muhimu kuzingatia kwamba kufunga kwetu kunatakiwa kusiwe kwa ajili ya manufaa ya sisi wenyewe ili kupata tamaa zetu za kimwili, au kwa kufuata mipango yetu wenyewe. Wakati wa kufunga ni wakati wa kutafakari, na ni wakati wa ukweli. Mungu hataheshimu kufunga ambako kunatokana na tamaduni za kidini tu na ambako kunafuata taratibu za kibinadamu. Ndiposa Mungu aauliza swali lingine katika Zekaria 7:5-7, "Hapo mlipofunga na kuomboleza . . . mlinifungia mimi?" Watu hawa walikuwa wakifunga lakini walikuwa wangali wakiishi katika hali ya kutotii. Ibada zao zilikuwa zenye unafiki kama ambavyo ilivyo hata katika siku zetu, wakati ambapo watu wanafunga lakini wangali hawamtii Mungu katika sehemu nyingi za maisha yao. Huku ni kufunga kama Mafarisayo, wakati mtu akitafuta utakatifu wake binafsi.

"Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi" (Mathayo 6:16-18).

Ni Ujuzi wa Kibinagsi

Kufunga ni ujuzi wa kibinagsi, haijalishi ikiwa mtu amefunga kutokana na uamuzi wake binafsi, au hata ikiwa amefunga kwa makubaliano na kundi fulani. Ikiwa tutakuwa na roho safi na mwelekeo unaofaa na wa wastani kuhusiana na miili yetu kama hekalu la Mungu, kufunga na kuomba ni jambo ambalo litakuwa na manufaa makubwa kama inavyodhahirika katika Agano Jipyia na Agano la Kale. Je, kuna uwerekano kwamba kama watu wa Mungu watamtafuta kwa bidii zaidi, na kukosa kukoma kufanya hivyo, na kwa kutumia njia ya kufunga na kuomba, kutakuwa na uwerekano wa nguvu za Mungu kudhahirishwa zaidi kwetu? Je, kuna hali ya kushindwa maishani mwetu ambayo itabadilika na kuwa ushindi? Je, kuna magonjwa ambayo yataponywa? Je, kuna maswali ambayo yatajibowi? Je, kutakuwa na ishara zaidi, na umwagikaji zaidi wa upako wake Mungu?

"Lakini hata sasa, asema Bwana, nirudieni mimi kwa miyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuomboleza; rarueni miyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana yeze ndiye mwenye neema, amejaah huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwangi wa rehema, naye Hughairi mabaya" (Yoeli 2:12-13).

Bwana harusi hayupo nasi tena katika mwili, na ni wakati wa wanafunzi wake kufunga! ■

Maswali na Majibu

Je, mtu anastahili kufunga kwa njia gani na kwa muda gani?

Huu ni uamuzi mwine ambao mtu anastahili kufanya kati yake na Mungu, kwa maana kufunga ni kipawa cha mtu kujitoa kibinasi.

Iwapo ni kufunga kwa njia ya kawaida, au kufunga kabisa kabisa, au hata kufunga nusu-nusu, aina hizo zote za kufunga zinahitaji kufanya kulingana na mwongozo wa Roho Mtakatifu na kwa ajili ya utukufu wake Mungu. Hata uamuzi wa mtu atafunga kwa muda gani ni jambo ambalo linategemea mwongozo wake Bwana. Musa, Eliya, na Yesu wamenakiliwa kwamba walifunga kwa siku arobanne, lakini kufunga huko kulikuwa kwa kutumia nguvu za kiungu, na ni jambo ambalo si la kawaida kwa mtu wa kawaida. Basi kufunga kwa muda mrefu sana ni jambo ambalo linastahili kufikikiriwa kwa makini, na kwa kutilia maanani afya yake mtu.

Je, mtu anastahili kufunga mara ngapi?

Agano Jipya halijatupatia miongozo ya Mkristo anastahili kufunga mara ngapi. Kutoka Luka 18:11-12 inaonekana kwamba Wayahudi walikuwa wakifunga mara mbili kwa wiki. Lakini kufikia wakati wa Kristo, Mafarisayo walikuwa wamefanya kufunga liwe ni jambo la kufunga watu kisheria. Lakini kuna mawaidha bora sana yanayopatikana katika Wagalatia 5:18: "Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria." Basi tunahitaji kuongozwa na Roho ili tujue ni mara ngapi tunastahili kufunga. Kuna hatari kwamba jambo la kiroho likifanya mara nyingi linabadilika na kuwa la mazoea tu, ambamo ndani mwake hamna roho. Lakini ikiwa kufunga kutafanyika kwa mara moja au zaidi, hili ni jambo la mtu kuamua kibinasi, pamoja na Mungu wake. Hili si jambo la mtu kufuata utamaduni wa kanisa, au jambo la lazima. Kuna watu ambao wameadhiri afya

Mfalme mmoja ananakiliwa kwamba alifunga kwa usiku mmoja kwa ajili ya Danieli (Danieli 6:18), kwa maana huo ndio hasa wakati ambapo hitaji hilo lilikuwako. Esta naye alifanya Wayahudi wafunge kwa siku tatu—mchana na usiku (Danieli 6:18). Na inavyoonekana kutoka kwa Maandiko kufunga kwa kawaida ambako Wayahudi walifanya ilikuwa ni kwa siku moja—kutoka wakati juu lilipokucha hadi lilipokuchwa (Waamuzi 20:26; 2 Samueli 3:35). Wakati huo chakula kililiwa jioni kabisa. Kufunga kwingine (nako) kulikuwa kwa masaa 24, kutoka kuchwa hadi kuchwa. Hata kuna wakati ambapo mtu anaweza kufunga chakula cha wakati mmoja tu (asubuhi/mchana/au usiku) ili aweze kutoa muda huo kumtafuta Bwana.

Kufunga ni mtu kuweka kando chakula cha kidunia ili ale chakula cha kiroho. Basi haifaai kwa vyoyote vile mtu kuweka kando chakula cha wakati fulani, halafu ikifika saa zingine za kula mtu ale chakula kingi zaidi. Lakini kilicho muhimu zaidi ni roho ya mhusika, roho ambayo imeshikamana na Bwana. Basi kufunga kunastahili kuwe kumetokana na Mungu ili mtu aweze kumheshimu na kumtukuza Yeye, na lengo la kufunga linastahili kuw ni kutimiza mapenzi yake Mungu kama Mfalme wetu.

yao kwa ajili ya kufunga mara nyingi na kwa kipindi kirefu zaidi. Jambo kama hilo halilingani na mafundisho ya kwamba Mkristo anastahili kuwa na kiasi, na ni mtu kukosa kutunza vizuri mwili wake ambao ni hekalu lake Mungu.

Pia ni jambo bora (sisi) tumtafute Mungu kwa dhati kwa njia ya kufunga na tusipuuzilie mbali manufaa na umuhimu wa kufunga. Yesu alisema kwamba wanafunzi wake watafunga, na hii ni kumaanisha kwamba ikiwa sisi kwa kweli ni wanafunzi wake, tunastahili kuwa tukifunga. Wakati mwine ambayo kufunga utatokana na mahitaji ya wakati huo. Basi kuna umuhimu wa mtu kutenga wakati wa wiki, au wa mwezi, ili afanyishe kazi nidhamu za kiroho maishani mwake na kujizitoa kwa Bwana kwa njia ya kuomba na kufunga.

Kuingizwa Kwenye Tafsiri za Biblia Maneno Ambayo Hayakuwemo Mbeleni

Kuna jambo la kuingiziwa maneno ambayo hayakuwemo (hapo) mbeleni katika sehemu zingine za tafsiri kadhaa wa kadhaa za Biblia. Katika baadhi ya tafsiri za Biblia kumetajwa neno kufunga katika Mathayo 17:21, Marko 9:29, na 1 Wakorintho 7:5. Lakini inaanminika kwamba kutajwa kwa neno hilo katika tafsiri hizo ni tendo la kuingizwa kwa neno baadaye, neno ambalo halikuwa katika nakala za kwanza za Biblia.

Mathayo 17:21 na Marko 9:29 zinasema kwamba wanafunzi walishindwa kumtoa pepo, naye Yesu akawaambia, "Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga." Kulingana na mchananu Adam Clarke na wachanganuza wengine, aya ya Mathayo 17:21 haiko kwenye "Nakala ya Vatican ambayo ni ya kitambo kabisa na ambayo hasa inaanminika sana karibu ulimwenguni kote." Andiko hilo pia limeachwa nje na nakala zingine za zamani ambazo ni za kutegemewa. Hata ingawa nakala fulani zina neno "kufunga" katika andiko la Marko, nakala ya Vatican haina neno hilo "kufunga", nayo Biblia ya Amplified inatumia italiki inaposema "na kufunga," na tafsiri

nyingine nyingi hazikubali uhakika wa neno hilo katika andiko hilo. Basi ushahidi wa kuwekwa kwa aya hiyo hakujahakikiwa. Ni jambo la kuzingatia kwamba Biblia za lugha zote ambazo zinatumika kutafsiri gazeti hili hutumia neno kufunga katika andiko hilo la Mathayo. Lakini tafsiri ya Kiswahili haitumii neno kufunga katika andiko la Marko.

1 Wakorintho 7:5 inasema kuhusu waume na wake zao kujitenga mmoja kwa mwine ambayo kwa ajili ya kutenga wakati wa kufunga na kuomba. Lakini neno 'kufunga' haliko kwenye nakala za kale kabisa, na hata watafsiri wengine hawatumii neno hilo katika andiko hilo. Kwenye kitabu chao wachanganuza wa mambo ya Biblia wanaojulikana kama Jamieson, Fausset, na Brown, wanasema kwamba matumizi ya neno "kufunga" hapo ilikuwa ni "kuingizwa mambo mapya mageni na wakristo wa kale ambao walipenda kufuata mafundisho ya kujinyima." Pia ni muhimu kuzingatia kwamba tafsiri za Kihispania na za Kiswahili hazina neno kufunga katika andiko hilo, ingawa linapatikana katika tafsiri za Kizungu na za Kijerumanii.



JE, WAJUA?

Katika makanisa (ya kawaida) ya Kikristo wakati wa Kwaresima (Lent) ni wakati spesheli wa maombi, kufunga, toba, kutoa sadaka, na kufanya matendo mema ili kuijandaa kwa ajili ya kusherehekeea kufufuka kwake Yesu. Lakini Kwaresima, ambayo hufanywa kwa siku arobanne, si jambo ambalo linatokana na mafundisho ya Biblia. Madhehebu mengine hutilia mkazo swala la kufunga katika wakati wa Kwaresima kama ukumbusho wa jinsi Kristo alivyofunga siku arobanne jangwani. Lakini jambo hili halilingani na mazoea ya kanisa la kwanza. Ingawa hivyo, kuna ushahidi kwamba kanisa la kwanza lilifunga kwa masaa karibu arobanne, masaa ambayo Yesu alikuwa kaburini—lakini hata jambo hili linazua majadala

mkubwa kutokana na maandishi ya kwanza ya kanisa. Kuna wahubiri wengine ambaao walifundisha kwamba watu walistahili kufunga kwa siku moja, ilhali wale wengine wakisema jambo hilo lilitahili kufanywa kwa siku mbili n.k. lakini jinsi ambavyo Kwaresima ilizinduka na kuendelea katika Kanisa ni jambo ambalo halina uhakika, ingawa mazoea yake yalitiliwa nguvu kupitia kwa ule Mkutano Mkuu wa Kanisa wa Nicaea, hapo mwaka wa 325 BK (Baada ya Kristo). Basi masaa hayo arobanne yalibadilika na kuwa siku arobanne za kufunga, lakini neno kufunga liliwekwa huru na kuhususishwa na mambo ya mtu kujinyima zaidi ya chakula.

Lakini watu wa Mungu hawako kwenye minyororo ya ujinga na utumwa wa dini za kibinadamu; badala yake watakatifu wa Mungu wanastahili kuishi maisha ambayo yanazidi kutolewa mhanga kwake Mungu.



KUMSIHI MUNGU

Musa akamsihi sana Bwana, Mungu wake . . . — Kutoka 32:11

Wakati Musa alipata sheria kutoka kwake Mungu katika mlima Sinai, na baadaye akashuka kutoka mlimani, alipata kwamba watu wake walikuwa wamemwacha Mungu, na sasa walikuwa wakiabudu sanamu ya ndama wa dhahabu. Basi hasira zake Mungu zikapanda na akamwambia Musa kwamba Yeye angewangamiza watu hao. Lakini Musa akamlilia Bwana wake na kumwomba aonyesha rehema zake ili abadilishe kauli na kuachana na hasira zake.

Kwa sababu Musa alinyenyekea mbele zake Bwana na kuomba rehema na msamaha wake, Mungu alibadili kauli na kuwaokoa wana wa Israeli. Ingalikuwa kama kwamba Musa hangemsihi Bwana kwa dhati ili apungunze hasira zake, wana wa Israeli wangeangamizwa, na Mungu angeanzisha taifa jipya kutokana na uzao wake Musa.



Njia za Mungu ni kamili na ni za haki, lakini Yeye hutenda mambo kwa rehema wakati ule watakatifu wake wanaliitia jina lake. Kuna wakati mwangi ambapo Mungu amebadilisha kauli lake na kubadilisha mfululizo wa mambo ya kawaida humu duniani kwa sababu mtu fulani amemtafuta.

Mungu anaheshimu maombi na kufunga kwa watu wake. Yeye huguzwa katika kitie chake cha enzi wakati watakatifu wake wanamwita ili awape msaada na ili aweze kuingilia kati kwenye mambo yao. Hata anapotangaza hukumu dhidi ya watu waovu Mungu hunyoosha mkono wake wa rehema na kuchilewesha hukumu zake wakati “Musa” (wa aina moja au nyingine) anapomsihii kufanya hivyo. Huu hasa ndio umuhimu wa maombi ya kumsihi Mungu. Adui yetu angetaka tufikirie kwamba litakalofanyika halina budi kufanyika, watu waombe au wasiombe. Lakini matukio ya jadi na ya kisasa yanadhihirisha kwamba Mungu akiwa huko Mbinguni husikiliza maombi ya watu wake. Basi hebu tuombe na tusichoke. Hebu tuweke umuhimu na tuwe tayari kulipa gharama ya kuomba huku tukijua kwamba jambo hilo halitatutuvutia tu kwake Mungu, bali pia linaweza kuleta utofauti katika maisha ya mtu aliyepotea, wakati Mungu akichelewesha hukumu zake kwa sababu ya maombi ya mmoja wa watoto wake waaminifu. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA